# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA SITA

**07 NOVEMBA, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 07 NOVEMBA, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 37 la tarehe 16 Septemba, 2022;
2. Toleo Na. 38 la tarehe 23 Septemba, 2022;
3. Toleo Na. 39 la tarehe 30 Septemba, 2022;
4. Toleo Na. 40 la tarehe 07 Oktoba, 2022;
5. Toleo Na. 41 la tarehe 14 Oktoba, 2022;
6. Toleo Na. 42 la tarehe 21 Oktoba, 2022; na
7. Toleo Na. 43 la tarehe 28 Oktoba, 2022.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Kutofuata Maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**66. MHESHIMIWA CONCHESTER LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Wazee watapata nafasi ya uwakilishi Bungeni kama ilivyo kwa Vijana na Wanawake ili waweze kusikilizwa na kutoa ushauri.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**67. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMAN BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga uzio na uwanja wa michezo katika Shule maalum ya Watoto wa Kike Asharose Migiro iliyopo Wilayani Mwanga.

**68. MHESHIMIWA JEREMIAH MRIMI AMSABI (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Hospitali ya Wilaya ya Serengeti na Nyerere DDH kwa kuzijengea uwezo wa kutoa huduma bora.

**69. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wataongezewa posho kama ilivyo katika Halmashauri nyingine nchini.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**70. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA (MTAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni kwa kiwango gani Mbunge anashirikishwa katika miradi inayoibuliwa na Wananchi katika Jimbo lake kupitia TASAF.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

**71. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Vikao vinavyopokea na kujadili changamoto za Muungano bado vipo na lini vilikaa mara ya mwisho.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**72. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kuiwezesha TASAC iweze kuhudumia meli nyingi.

**73. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Simiyu utaanza baada ya kukamilika zoezi la uthamini wa eneo la Uwanja utakapojengwa.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**74. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, nini mpango wa Serikali kuwasikiliza na kufanyia kazi hoja za Wamachinga hasa baada ya zoezi la kuwapanga.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**75. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (CHAANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa Kituo kidogo cha Polisi cha Chaani Lungalunga.

**WIZARA YA AFYA:**

**76. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya uhaba wa Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa.

**WIZARA YA MADINI:**

**77. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wanawake wanakuwa wachimbaji wa Madini nchini.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**78. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mkakati gani wa kuzuia nyavu haramu.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**79. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, ni upi mchango wa Serikali Kuu katika ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa Michezo wa Halmashauri ya Mji wa Geita.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**80. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Askari Wanyamapori katika Wilaya ya Itilima na maeneo yanayozunguka Pori la Akiba Maswa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**81. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itaanza programu ya kuunda na kurusha setelaiti angani.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**82. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha upatikanaji wa soko la Machungwa.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**83. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Mahakama ya Wilaya Korogwe itajengwa.

## WIZARA YA KILIMO:

**84. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGIDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itawatafutia Wakulima wa Kishapu masoko ya mazao ya Mtama na Uwele.

**85. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za Alizeti kwa Wakulima ili kuzalisha mafuta ya kula.

**86. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha pembejeo za Korosho kwa msimu wa Mwaka 2022/2023 zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Kutofuata Maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## V. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **07 NOVEMBA, 2022** | **KATIBU WA BUNGE** |